**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**

TPHPA

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# TANGAZO KWA UMMA

**04 Februari, 2026**

## MAKAMPUNI YA TANZANIA YALIYOPATA USAJILI WA MAMLAKA KUU YA FORODHA YA JAMHURI YA WATU WA CHINA NA KURUHUSIWA KUSAFIRISHA MAZAO YA KILIMO KWENDA CHINA

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) inapenda kuutaarifu umma, wadau wa sekta ya kilimo na biashara, kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Kilimo, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushrikiano wa Afrika Mashariki, Ubalozi wa Tanzania nchini China na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, imefanikiwa kuratibu na kuwezesha usajili wa **Makampuni 408** ya Tanzania katika Mfumo wa Mamlaka Kuu ya Forodha China ***General Administration of Customs of China*** (GACC) na kuruhusiwa kusafirisha mazao mbalimbali ya kilimo kwenda soko la China. Idadi ya Makampuni imeorodheshwa kwenye Kiambatanisho cha taarifa hii.

Usajili huu ni sehemu ya utekelezaji wa masharti ya ***Sanitary and Phytosanitary Measures*** **(SPS)** na makubaliano ya kibiashara kati ya nchi hizi mbili, unaolenga kuhakikisha kuwa mazao yanayosafirishwa yanakidhi kikamilifu matakwa ya Afya ya Mimea, ubora na usalama wa chakula yanayotakiwa na soko la China.

**Mamlaka inapenda kusisitiza kuwa:-**

i. Makampuni yote yaliyosajiliwa yanapaswa kuendelea kuzingatia *masharti ya usimamizi wa afya ya mimea*, ufuatiliaji (traceability), matumizi sahihi ya viuatilifu na taratibu za ukaguzi kabla ya usafirishaji;

ii. Makampuni yanayopenda kusafirisha bidhaa za kilimo kwenda nchini China yanapaswa kuwasilisha maombi TPHPA (kwa email; dg@tphpa.go.tz) kwa ajili ya mwongozo wa taratibu za kulifikia soko la China kupitia mfumo GACC.

iii. Mamlaka inatoa wito kwa wadau wote kuendelea kushirikiana na kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuhakikisha Tanzania inanufaika kikamilifu na fursa za soko la China ambalo litaiongezea nchi mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi, kukuza uchumi wa wakulima na kuchangia pato la taifa.

iv. TPHPA itaendelea kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha uzingatiaji wa masharti ya kitaifa na ya nchi lengwa yanafikiwa.

TPHPA inapenda kutoa shukurani nyingi kwa Uongozi wa Wizara ya Kilimo kwa kuiwezesha Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania ili kuyafikia masoko ya nchi ya China. Aidha TPHPA inaahidi kuendelea kufungua masoko ya bidhaa za kilimo kwenye nchi nyingine duniani ili kutanua wigo zaidi wa bidhaa za kilimo kutoka Tanzania ikiwa ni mchango wa TPHPA wa utekelezaji wa Ajenda 10/30 ya Wizara ya Kilimo.

**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA)**

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY
P.O. Box 3024, Tel.: +255 27 297 0487
ARUSHA - TANZANIA